

TAARIFA YA PAMOJA KWA VYOMBO VYA HABARI

Katibu Mkuu Msaidizi wa Umoja wa Mataifa na Mratibu Mkuu wa Mpango wa Utoaji Chanjo ya Uviko-19 azuru Tanzania

Dodoma, Julai 6, 2022 – Bw. Ted Chaiban, ambaye ni Katibu Mkuu Msaidizi wa Umoja wa Mataifa na Mratibu Mkuu wa Mpango wa Utoaji Chanjo ya Uviko-19 (CoVDP), yupo nchini Tanzania kwa ziara maalumu ya siku nne. Miongoni mwa matukio muhimu katika ziara yake ni mkutano wake wa jana na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Philip Isdor Mpango ambapo kwa pamoja walijadiliana mikakati ya kuongeza kasi ya utoaji chanjo ya UVIKO-19 nchini Tanzania ili nchi ifikie malengo yake ya kuchanja wananchi.

Katika ziara yake hii, Bw. Chaiban pia amekuwa akifanya mikutano na viongozi wengine wa ngazi za juu Serikalini, washirika wa maendeleo, asasi mbalimbali, viongozi wa dini na wadau wengine muhimu.

“Ninaipongeza Serikali kwa juhudi inazofanya katika kuhamasisha chanjo dhidi ya UVIKO-19. Niko hapa ili kutathmini hatua ambayo Tanzania imepiga katika kufikia malengo yake ya utoaji chanjo na kujadiliana njia za kukabiliana na vikwazo na kupanua program ya utoaji chanjo,” alisema Bw. Chaiban. Alikuwa akizungumza katika mkutano wa pamoja na Waziri wa Afya, Mh. Ummu Mwalimu, Waziri wa Fedha na Mipango, na Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa).

Bw. Chaiban alisisitiza kwamba janga la UVIKO langalipo na kwamba hatari ya kuibuka aina mpya ya virusi, hasa kwa makundi ambayo bado hayajapata chanjo, ingali kubwa. “Janga la UVIKO-19 bado lingali kati yetu na hatuna budi kuhakikisha

kwamba tunawalinda wale walio hatarini zaidi, wakiwemo wazee, watu wenye maradhi sugu, watumishi wa afya walio mstari wa mbele na wale wanaofanya kazi katika sekta za utalii na hoteli. Chanjo ndiyo kinga yetu madhubuti dhidi ya UVIKO-19. Hakuna aliye salama hadi sote tuwe salama. Kama wanavyosema katika Kiswahili: 'Ni ujanja kuchanja'!

Bw. Chaiban aliteuliwa kuwa Katibu Mkuu Msaidizi wa Umoja wa Mataifa na Mratibu Mkuu wa Mpango wa Utoaji Chanjo ya Uviko-19, mwezi Februari, 2022 na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa António Guterres.

###

Maelezo kwa Wahariri:

Taarifa Mpya kuhusu Chanjo ya UVIKO-19

Hadi mapema mwezi Julai, 2022, karibu dozi bilioni 12.1 za chanjo za UVIKO-19 zilikwishatolewa kote duniani. Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), asilimia 61.6 ya idadi ya watu ulimwenguni wamekwishakamilisha chanjo lakini ni asilimia 13 tu ndio wanatoka katika nchi za kipato cha chini. Kanda za WHO za Afrika na Mashariki mwa Bahari ya Mediterranean zina idadi kubwa zaidi ya watu ambao bado hawajapata chanjo. Nchini Tanzania, program ya chanjo za UVIKO-19 ilianza 28 Julai 2021. Takribani Watanzania milioni 10 tayari wamepata chanjo, walau dozi moja na watu 8,553,930 (13.96%) wamepata chanjo kamili hadi hivi sasa.

Kuhusu Ted Chaiban

Ted Chaiban amekuwa na historia ya kutukuka katika Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF). Amefanya kazi kama Mkurugenzi wa Kanda ya Mashariki ya Kati na Afrika ya Kaskazini tangu mwezi Oktoba, 2019. Kabla ya jukumu hilo, alikuwa Mkurugenzi wa Programu wa UNICEF (2014-2019), Mkurugenzi wa Programu za Dharura (2012-2014), Mwakilishi wa UNICEF nchini Ethiopia (2009-2012), nchini Sudan (2005-2009) na Sri Lanka (2002-2005). Kwa maelezo zaidi kuhusu maisha yake, soma [hapa](#).

Kuhusu Mpango wa Ushirika wa Utoaji Chanjo za UVIKO-19 (CoVDP)

Mpango wa Ushirika wa Utoaji Chanjo za UVIKO-19 (CoVDP) ni mradi wa mashirika mbalimbali uliozinduliwa na UNICEF, WHO na Gavi mwezi Januari 2022 ili kusaidia nchi 92 za AMC katika kuongeza kasi ya utoaji chanjo, kwa kuweka msisitizo wa kipekee kwenye nchi 34, Tanzania ikiwemo, ambazo zilikuwa chini ya asilimia 10 ya lengo kufika mwezi Januari, 2022.

Kwa Mawasiliano Zaidi kwa Vyombo vya Habari:

- Edgar Kiliba, Mchambuzi wa Mawasiliano, Ofisi ya Mratibu wa Umoja wa Mataifa nchini Tanzania, Barua pepe: edgar.kiliba@un.org | Simu: +255 692 890 077
- Nisha Schumann, Mnadhimu Mkuu (a.i.), UVIKO-19 Ushirika wa Utoaji Chanjo, Barua pepe: schumannn@who.int | Simu: +226 6186 2929